22070299

IB DIPLOMA PROGRAMME
PROGRAMME DU DIPLÔME DU BI
PROGRAMA DEL DIPLOMA DEL BI

**SWAHILI A1 – STANDARD LEVEL – PAPER 1**
**SOUAHÉLI A1 – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 1**
**SUAHILI A1 – NIVEL MEDIO – PRUEBA 1**

Monday 14 May 2007 (morning)
Lundi 14 mai 2007 (matin)
Lunes 14 de mayo de 2007 (mañana)

1 hour 30 minutes / 1 heure 30 minutes / 1 hora 30 minutos

---

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Write a commentary on one passage only. It is not compulsory for you to respond directly to the guiding questions provided. However, you may use them if you wish.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Rédigez un commentaire sur un seul des passages. Le commentaire ne doit pas nécessairement répondre aux questions d'orientation fournies. Vous pouvez toutefois les utiliser si vous le désirez.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Escriba un comentario sobre un solo fragmento. No es obligatorio responder directamente a las preguntas que se ofrecen a modo de guía. Sin embargo, puede usarlas si lo desea.


© IBO 2007

*Toa maoni yako juu ya* ***moja*** *ya tungo zifwatazo.*

**1.** (a)

Hadhari ubaraguzi, mke ni fingo la nyumba
Sijitie ubabazi, kila kiutu ukafumba
Utamkausha ngozi, mke ni kama mgomba
Mke ni fingo la nyumba, hadhari kumchezea

Simtie simanzi, pa kheri kutia miba
mke akawa hawezi, chakula tabu kushiba
Mke ni kama ndizi, huhitaji rutuba
Mke ni fingo la nyumba, hadhari kumchezea

Usimfanye kitwazi, mzigo yako hubeba
Ukamkausha nguzi, neno akawa jembamba
Mke sio mpangazi, au nakao wa shamba
Mke ni fingo la nyumba, hadhari kumchezea

Mpe mema maikazi, mema ya ambao kwamba
Na awe ndiye mlazi, kiticho katika nyumba
Siyo wende matembezi, umwache kinywa chafumba
Mke ni fingo la nyumba, hadhari kumchezea

Mfanye ukiwuezi, mke mfanyue suhuba
Na kumpa maungezi, mazuri katika huba
Awe ni msumizi, wa furaha si msiba
Mke ni fingo la nyumba, hadhari kumchezea

Muweke matumizi, sanaa zisiwe haba
Jitume ufanye kazi, mke apate kushiba
Na ukifikia mwezi, na ujipambe si haba
Mke ni fingo la nyumba, hadhari kumchezea

Umpe mema malezi, atume katika nyumba
Awe nao vijakazi, na vitwana kumpumba
Msabiliye ghawazi, atumie kujiramba
Mke ni fingo la nyumba, hadhari kumchezea

Kumchezea maizi, mtunze mfano shamba
Mpambe kwa vidairizi vya dhahabu kumbuka
Na kama hivyo huwezi, mpambe japo kwa shaba
Mke ni fingo la nyumba, hadhari kumchezea

Mfanye ndugu mpenzi, mfanye kwako ni tiba
Nenda naye matembezini, kama pesa ni mkoba
Mfanye awe hirizi, au cha lulu kikuba
Mke ni fingo la nyumba, hadhari kumchezea

Na fupiza beti hizi, ndugu kwenu nawaamba
Nawaamba wasikizi, wake muwape vilemba
Dhari wewe azizi, moyoni wewe ni hiba
Mke ni fingo la nyumba, hadhari kumchezea

Angila Jane Obando, *Mwongozo wa mashairi* (2005)

– Mwandishi anateua na kutumia maneno yake kivipi ili kufanikisha mtindo wa shairi lake.

– Muundo anaotumia mwandishi unasaidia kwa njia gani ili kuelewa shairi lake.

– Ni kwa njia gani mwandishi ameathiri msimamo wako kuhusu swala analozungumzia.

**1.** (b)

**Hakuna mume wa waume**

Kasoro alikuwa barobaro jamali. Haiba yake ilivutia wengi hususan lile tambo lake la juu lililomfanya kuonekana kama bingwa wa masumbwi ya uzani wa juu. Alitembea kwa mikogo na madaha huku ametanua kifua mithili ya belewasi katika msitu wa Abadare. Kasoro alikuwa na misuli iliyotutumka na aliyopenda kuiweka wazi kwa lengo la kuwaogofya vijana wenzake. Maungo ya mbabe huyu yalitoa hadhari ya wazi bila haja ya kuandikwa 'gusa uone' mgongoni.

Watu wenye nguvu aghalabu husheheni tadi, kiburi na majipato. Hili halikuwa baidi na hulka za kasoro, chambilecho wahenga, kizuri hakikosi ila. Kesi chungu nzima za vijana kugotwa, kuzabwa makofi na hata kunyanyuliwa hobelahobela na kisha kubwagwa ziliwasilishwa nyumbani kwa kina Kasoro. Wazazi wake walimpa nasaha kwa kumhubiria upole, urafiki na upendo kwa shababi wenzake lakini hayo yote yalikuwa yakiingilia sikio moja na kutokea la pili. Kasoro alikuwa ameyatia masikio yake kokwa.

Siku moja mkota huyu alitiwa chuoni akakomolewa majigambo yake. Kweli hakuna marefu yasiyokuwa na ncha.

Siku hiyo alfajiri na mapema Kasoro aliabiri matwana ya kuelekea mjini. Pale kitini alipoketi alikataa katakata kufunga mkanda wa usalama garini. "Ndugu abiria fungeni mikanda." Kondakta aliwasihi abiria wake.

Kasoro alimtolea jicho la bezo na kujibu kuwa hilo halikuwa na umuhimu wowote. Akaongeza kwa dhara "Hii tabia ya mtu kujifunga hatamu Kama ng'ombe ni ya nini? Kama polisi hawana kazi ya kufanya ila kukagua mikanda, waambieni waje tuwape kazi ya kukamua ng'ombe."

"Hatufungi mikanda kwa ajili ya polisi, ila kwa sababu ya usalama wetu" alimjibu mojawapo wa abiria. Haya yalimghadhabisha kasoro si haba. Alilivua shati kuonyesha misuli yake. Abiria wakahofia kuwa ukimfukuza sana mjusi atageuka nyoka. Wakafyata ulimi. Baada ya kusafiri kwa muda, walifika kwenye kizuizi cha barabarani. Askari alilipungia mkono gari kuliashiria lisimame. Inspekta akamhoji dereva, mbona abiria wako mmoja hajafunga mkanda?" Dereva alikawia kujibu, hatimaye akaona kwamba 'ukimficha jogoo pakachani kuna wakati atawika. Akaamua kusema ukweli. Alimweleza inspekta kuwa abiria huyo alikuwa amekataa kufunga mkanda kwa makusudi. Polisi walimtaka kasoro ashuke. Kasoro naye akadinda huku akijitanua kifua na kufurisha misuli, ungedhani alikuwa anajitayarisha kwa pambano la miereka.

Anayetaka kuwa kibogoyo anikaribie!" alinadi Kasoro. Inspekta hakufanya ghamidha bali aliingia katika gari hilo na kumwamuru dereva alipeleke hadi kituo cha polisi. Dereva alisalimu amri. Kama wa dhihaki tu Kasoro alitanabahi amefikishwa kituo cha polisi. Mara askari wakalizingira gari mithili ya nzige wanavyolivamia tawi la mti.

"Utashuka kwa salama na amani au hushuki?" alikuli inspecta.

Kasoro akaona kuwa 'ogopa ni ngao pia'. Heri kushuka kuliko kujitakia balaa bure.

"Kijana jizoeze kunyoosha miguu kadiri ya kitanda chako. Ulijifanya una nguvu, utawaweza hawa?" Inspecta alimsaili Kasoro.

Kasoro alifikishwa mahakamani akikabiliwa na shtaka la kuvunja mojawapo ya sheria za barabarani. Alipatikana na hatia na akahukumiwa na akatozwa faini ya shilingi elfu mbili lau sivyo afungwe miezi miwili. Alikuwa amewamba na kwa kukosa pesa za faini alikula kalenda ya miezi miwili.

Baada ya kutumikia kifungu chake, kasoro alielewa maana ya kutumikia kifungu chake. Kasoro alielewa kuwa, hakuna mume wa waume.

*Kiswahili kwa kidato cha nne*, Kenya literature bureau (2005)

- Toa maoni yako kuhusu nafasi ya Kasoro katika kifungu hiki.
- Mwandishi wa kifungu hiki ana shauku ya kupitisha ujumbe gani?
- Mwandishi anaonyesha umuhimu gani wa mazungumzo na maelewano.
- Mwandishi anaamsha na kunasa hisia za wasomi wake kwa njia gani?